

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI

10 JUNI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 10 JUNI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**345. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inaonyesha kwamba asilimia 7 ya Watanzania wanaishi Vijijini lakini katika miaka ya hivi karibuni watu wengi hasa Vijana wanakimbilia Mijini wakidai kuwa maisha ni magumu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza au kudhibiti hali hiyo.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

346. MHESHIMIWA JANET MAURICE MASABURI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi zikiwemo Bahari, Maziwa, Mito na Mabwawa mengi ya asili pamoja na rasilimali watu kubwa ambao hawana ajira:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Vijana na Akina Mama kwenye kila Halmashauri nchini kutenga maeneo maalum ya kujenga Mabwawa ya kufugia Samaki ili makundi hayo yapate kujijiri.

WIZARA YA KILIMO:

347. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Eneo la Mbuga linalozunguka Mji wa Itigi linafaa sana kwa kilimo cha mazao mbalimbali kama Mahindi, Alizeti, Choroko na Dengu lakini eneo hili linajaa maji na kufanya Kilimo kuwa kigumu:-

Je, Serikai ipo tayari kusaidia Wananchi wanaolima katika eneo hilo kwa kuwajengea mifereji ya kuongoza maji yasiingie mashambani.

WIZARA YA NISHATI:

348. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa ulipwaji fidia kwa Wananchi zaidi ya elfu mbili (2000) wa Wilaya za Longido na Monduli ambao maeneo yao yalipitiwa na Mradi wa Umeme Vijijini (REA).

349. MHESHIMIWA JUSTIN JOSEPH MONKO (SINGIDA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Jimbo la Singida Kaskazini limepata Mradi wa Umeme Vijijini (REA na BTIP) ambapo utapeleka umeme katika Vijiji 54 kati ya 84; katika baadhi ya maeneo ambayo mradi umepita umeacha nyumba za Wananchi, Taasisi za Dini, Taasisi za Serikali na pampu za maji pasipo kuziunganishia umeme :-

(a) Je, Serikali ina kauli gani kwa maeneo hayo yaliyorukwa na Wananchi

walikwishafanya *wiring* kwa matarajio ya kuunganishiwa umeme;

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji 30 vilivyosalia;

(c) Je, Serikali ipo tayari kusaidia njia mbadala ya Umeme wa Jua (*solar power*) katika maeneo ya huduma muhimu kama Zahanati, Sekondari na huduma za maji wakati tukisubiri usambazaji katika Vijiji vilivyosalia.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

350. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kumekuwa na kero kubwa sana kwa abiria wanaotumia Bandari kwenda Zanzibar kwa Boti ambapo hulipishwa ushuru wa Bandari kwa mizigo hata boksi la kilo kumi tu au Mchele wa kg 20 kwa malipo ya Sh. 9,750/=:-

Je, ni mizigo gani ambayo abiria anapaswa kuilipia ushuru huo wa Bandari.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**351. MHESHIMIWA TASKA RESTUTA MBOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Mtoto mwenye ugonjwa wa *Sickle cell* hutakiwa kupata matibabu mfululizo ambapo kwa familia zisizo na uwezo hushindwa kulipia gharama za matibabu na hivyo kusababisha Mgonjwa kupoteza maisha:-

- Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wagonjwa wa *Sickle Cell* kupata matibabu bure.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**352. MHESHIMIWA ZUBEDA HASANI SAKURU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Ongezeko la gharama za nishati nchini hasa umeme na gesi vimesababisha kuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya kuni na mkaa:-

Je, ni lini Serikali itarasimisha biashara ya mkaa ili kupunguza makali ya maisha hasa kwa Watanzania wenye kipato duni.

WIZARA YA MAJI:

**353. MHESHIMIWA JEROME DISMAS
BWANAUSI (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Wananchi wengi wa Vijiji vya Miese, Utimbe, Naliongolo, Mtolya, Geuza na Mchoti wamekuwa wakiliwa na Mamba na wengine kujeruhiwa vibaya hasa wanapokwenda kuchota maji katika Mto Ruvuma kutokana na ukosefu wa maji katika maeneo yao:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuchimba visima vya maji katika Vijiji hivyo ili kunusuru Wananchi wanaouawa na kujeruhiwa na Mamba wanapofuata maji katika Mto huo.

**354. MHESHIMIWA MUSA RASHID NTIMIZI
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
Serikali ina mpango wa kuleta maji katika Mkoa wa Tabora toka Ziwa Victoria lakini Jimbo la Igalula halipo katika mpango huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Vijiji vya Jimbo la Igalula katika mradi huo.

**DODOMA
10 JUNI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**